
# Daktari Yesu

## Yesu Tafadhali Niponye



Imetafsiriwa na wafungwa wa Hong Kong

www.doctorjesus.org

## Mathayo 4 : 23 - 24

Yesu akaenda pande zote nzima ya Galilaya,
na kuhubiri katika nyumba ya ibada,
na kutangaza habari njema ya ufalme,
na kuponya magonjwa yote
miongoni mwa watu wagonjwa,
na kuwaleta wagonjwa na kuwaponya



*"Healed of Cancer" na Dodie Osteen,
kueleza vipi aliweza kutibu cancer ya ini
wakati akipewa wiki 3 ya kuishi mwaka 1981.
Yeye na mume wake, wote wachungaji,
waliomba na cancer ikatoka, kwa kutumia
maombi maalumu 40 katika Biblia.
Kitabu chake kilikuwa kinatia msukumo kwa
kila mtu ambae alikuwa anaugua cancer.
Inapatikana katika www.amazon.com*


Kwa muda wa miaka 5 sikuweza kunyanyua kuzunguka mkono wangu.
Na kuomba msaada kwa Yesu.
Na hivi sasa naweza kunyanyua, kuzunguka!
-Yeye ni mfungwa katika Hong Kong Dec 2011




Katika jela ya HK ndani wa mwezi Julai 2011,
niliambiwa kwamba mtoto wangu
anatarajiwa kuzaliwa mgonjwa.
Mimi na rafiki zangu alimwomba Yesu.
Mwezi wa Novemba 2011, daktari akaniambia
"mtoto wako atakua salama." Akazaliwa
wa kike mwenye afya njema
ndani ya mwezi Februari 2012!

Mathayo 8 : 5 - 13

Akida akaenda akamwambia Yesu, akasema "Bwana mtumishi wangu amelala nyumbani, ni mgonjwa sana na amepooza."
Akamwambia "Nitakuja na kumponya."
Akida akajibu "Hustahiki kuja nyumbani Bwana, wewe sema neno tu na mfanyakazi wangu ataponywa."
Yesu akajibu "Nenda myumbani kwako, na kuamini kwako ndio kumemponyesha."
Yule mfanyakazi wako ameshapona




*Yesu nifundishe maombi ya uponyaji*

01-12-2011 Mfungwa mmoja kutoka katika jimbo la Hunan nchini China, ambae yuko kizuizini Hong Kong, aliambiwa na daktari kwamba maini yake si mazuri, yafaa kubadilisha
09-01-2012 daktari kutoka Queen Elizabeth Hospital na Princess Margaret Hospital walisema maneno yale yale kwamba "unahitaji kubadilisha maini na utatayarisha matibabu haya utakapo rudi nyumbani kwenu."
12-01-2012 Mfungwa alirudi toka hopsitali, akiwa kizuizini, mchana wa January 27, alipokea kitabu cha "Daktari Yesu". Usiku ule alifanya maombi kwa Yesu. Matatizo yake yaliponywa. Baadae alifanyiwa uchunguzi zaidi wa afya yake na daktari alimwambia kwamba "matatizo yako ya ini yamepona."

---

Mfungwa mwengine alikuwa kizuizini katika Hopsitali hio. Kabla ya kuwekwa kizuizini mwaka 2006 alifanyiwa operesheni ya kuondoa mawe 30 katika figo lake. Aliwekwa kizuizini 2007. Mnamo mwaka 2011 matatizo yake ya figo yakamrejea ni. Katika mwezi wa Nov, 2011 aliambiwa baada ya x-ray kwamba figo lake jengine limeonekana na kuwa na jiwe moja jipya…..kwa hio anahitajika kufanyiwa operesheni nyengine. Kwa hio alimuomba Yesu msaada na baadae alijisikia nafuu na x-ray ilionyesha kwamba hana jiwe tena katika figo lake. Kwa hio hahitaji operesheni nyingine

## Mathayo 8 : 1 - 3

Mtu mwenye maradhi ya ukoma alikuja kwa Yesu, ameinamisha kichwa chake mbele ya Yesu akasema
"Bwana, kama unataka unaweza ukaniponya."
Yesu akanyoosha mkono wake na kumshika mwenye ukoma, na alisema, "Bilashaka nataka kukuponya, ponywa," na yule mkoma akapona




*Yesu hakuwahi kumkatalia mtu alietaka kuponywa kwake alimponya kila mtu alietaka kuponywa kwa hio ,inamaana wataka kuniponya na mimi kamwe*

*Yesu hakusema "ugonjwa huu ni mzigo kwako lazima ustahamili nao hivyo."*
*Yesu aliuchukulia ugonjwa, kama mzazi anavyochukulia ugonjwa kwa mwanawe, ni kitu ambacho kinabidi kishughulikiwe na kutibiwa haraka iwezekanavyo hakuna hata mtu mmoja ambae anataka mtoto wake kuumwa, tuna fanya makosa tuna posema Mungu anapenda mtu mgonjwa.*
*Huwa anapenda kama vile wazazi wanavyo wapenda watoto wao wasiwe wagonjwa*

Mathayo 8 : 14 - 15

Yesu alikwenda nyumbani kwa rafiki yake Peter. “Mama mkwe wake Peter” alikuwa mgonjwa. Yesu alimgusa mkono wake, na kupona. Alinyanyuka na kuanza kuwagawia chakula na maji




*Mfungwa alieko kizuizini Hong Kong. Alikua na matatizo ya maumivu ya kifua. Mnamo Nov 30, 2011 alifanyiwa uchunguzi na kugundulika na ana shimo katika mapafu ya upande ya kushoto. Alihamishiwa katika Queen Elizabeth Hospital mnamo Dec 8, alifanya maombi, usiku ule maumivu ya katoweka. Mnamo Dec 15, baada ya uchunguzi daktari alimwambia kwamba “Shimo limetoweka .....na anaweza kwenda!”*

Mathayo 8 : 16 - 17

Siku moja jioni wagonjwa wengi walipelekwa kwa Yesu wakaponywa. Habari hii ilihubiriwa na Isaya kipindi kirefu kabla ya Yesu kuzaliwa “anaponyesha watu”



*Mnamo tarehe Dec 04, 2011, Mfungwa mmoja alisimama kwenye maombi, na kuwataka wafungwa wenzake kufanya maombi kwa mfungwa mwenzao ambae hakuhudhuria kwa sababu ya kusumbuliwa na mgongo na kushindwa kutembea. Wafungwa walifanya maombi na kumpatia nakala ya kitabu cha “Daktari Yesu”. Baada ya siku kadhaa ya kupokea nakala ya kitabu hicho, alifanya maombi na akaweza kusimama na kutembea*

*Yesu, tafadhali chukua maradhi yangu.*
*Tafadhali chukua maumivu ya mgongo wangu*
*Tafadhali chukua kansa yangu*

## Mathayo 9 : 2 - 8

Mtu mmoja alipelekwa kwa Yesu, akiwa amebebwa kwenye machela, akiwa amepooza. Kwa kuona Imani yao, Yesu akamwambia yule mgonjwa "Amka, na uchukue kitanda chako na uende nyumbani," mgonjwa akaamka na akaenda nyumbani. Walipoona miujiza ile wakamtukuza Mungu kwa vile Yesu alivyofanya



*Mnamo Feb 05 2012, Mfungwa toka katika kizuizini kilichoko kisiwani alikuwa anatapika damu akapelekwa Queen Elizabeth Hospital kwa ajili ya uchunguzi na ikagundulikana kuwa ana tundu katika tumbo lake. Baada ya kupata matibabu hospitalini kwa muda wa siku 5, alipata afadhali. Mnamo Feb 10 baada ya kupokea kitabu cha "Daktari Yesu" na kuomba msaada wa Yesu. Baadae aliweza kulala vizuri bila maumivu yoyote. Feb 11 alipona maumivu yake, na Feb 12 daktari alimwambia "nenda nyumbani"*

## Mathayo 9 : 18 - 25

Viongozi wa dini walikuja kwa Yesu na wakasema "Binti yangu sasa hivi ameshafariki, njoo uweke mkono wako juu yake nae ataishi." Akaondoka Yesu akafuatana na wanafunzi wake.



Wakati yupo njiani, akakutana na mwanamke mmoja, alikuwa na ugonjwa wa kutoka damu kwa muda wa miaka 12 na kugusa upindo wa kanzu ya Yesu, kwa maana alisema moyoni mwake "nikigusa tu upindo wa kanzu yake nitapona." Yesu akamwambia "jipe moyo binti yangu, Imani yako imekuponya," yule mwanamke amepona toka saa ile.

Yesu alipofika nyumbani kwa yule mjumbe. Aliona wapiga filimbi wakifanya maombolezi, akawambia "ondokeni, huyu msichana hajafariki, bali amelala wakamcheka sana," waombolezaji walipoondoka Yesu aliingia na kumshika yule msichana, na yule msichana alisimama



## Hadithi kutoka America mnamo mwaka 1940, kutoka p. 48 ya "The Healing Light" na Agnes Sanford

Kijana mmoja alilazwa hospitali akiwa mahututi huku shangazi yake akiwa pembezoni mwa kitanda chake.
Siku moja jioni alimtaka Agnes pamoja na marafiki zake kumfanyia maombi, walimfanyia maombi mnamo saa tisa na mchana, wakimtaka shangazi kuweka wake juu yake.

Mnamo saa tisa na dakika 45, yule kijana alimuuliza shangazi yake Lucy "Kimefanyika nini juu yangu? Mara hii najisikia niko mzima na nimepona." Hospitalini waliamua kumuweka siku moja zaidi kwa ajili ya uchunguzi, na baadae na kukutwa "negative" au kukutwa salama. Tukio hili limetokea katika Baltimore Hospital. "Ni miujiza," daktari Alisema

Bwana Yesu,tafadhali nifundishe jinsi ya kuomba kwa ajili ya wagonjwa

Mathayo 9 : 27 - 33

Vipofu wawili walimwita Yesu,
“Tusamehe mtoto wa Daudi.”
Akawauliza “Mnaamini kwamba naweza kufanya?” Wakasema “ndio Bwana”.
Hapo akawagusa macho yao na akasema “Imani yenu imewaponya na wakaona.”
Muda mdogo baada ya kuacha nao, na baadae akaletwa bubu mwenye mashetani kwa Yesu na kuwatoa mashetani na baadae akaongea



## Mapendekezo Makubwa (see www.amazon.com)

F.MacNutt : Healing; The Healing Reawakening
A. Sanford : Sealed Orders; The Healing Light
E.Tardiff : Jesus is the Messiah
J. Girzone : Joshua

---

## Sababu 11 kwa nini watu hawaponyi alielezea katika "Healing" na F. MacNutt

1. Ukosefu wa Imani
2. Kuchanganyikiwa kuhusu ahadi za uponyaji
3. Kuchanganisha vitu vya uongo
4. Kutosa mehewa dhambi
5. Kukosa kuomba vilivyo
6. Kuto kutambua magonjwa
7. Kutotimiza maagizo ya daktari
8. Hawataki kutumia kwa uponyaji
9. Kusema muda haujafika
10. Kutumia mtu mwengine kama chombo cha uponyaji
11. Matatizo kushindwa kuyatatua

---

Yesu, kama haya maombi yangu ya uponyaji hayatafanyakazi, naomba unieleza kwa nini, au kama nitaweza kufanya kitu chochote ili niweze kuponya. Naomba unisaidie nipate uwezo wa uponyaji "ameni"

## Mathayo 9 : 35

Yesu alizunguka mjini na vijijini na kuhubiri katika majumba ya ibada na kutangaza habari njema za ufalme na kuponya magonjwa.



Q : Kama Mungu anataka niwe mzima, kwa nini niumwe ?

A : Wazazi wananitaka niwe mzina, sio mgonjwa, kama sitoangalia afya yangu, basi nitakua mgonjwa, na kwa hio sio makosa ya wazazi wangu.

Q : Vipi kuhusu wale watoto waliozaliwa wagonjwa ?

A : Mungu anatengeneza kila kitu kizuri na kipya kama computer, lakini pamoja na upya wake muda mwengine inaweza ikapata maradhi yaani “virus infected”, kwa hio inapopata maradhi bila ya kutegemea, kwa hio maradhi ya hapo ni kama Shetani kwa binadamu siku zote huwa anatusha wishi kutenda maovu, kwa hio muokozi mkubwawa Shetani ni Bwana Yesu. Yesu pekee ndie atatuponya.

## Mathayo 12 : 10 - 14

Yesu alifanya mkutano katika nyumba ya ibada, akaona mtu na aliyepooza mkono.
Yesu akamwambia "nyosha mkono wako." Yule jamaa akanyoosha mkono wake ukawa mzima




*Baba yake Gavana alikuwa mgonjwa na anaharisha, amelala kitandani, akaponyeshwa na Paulo kwa kumuwekea mkono wake na akapona. Neno lake la uponyaji lilipita kila sehemu katika mwili wake na akapona. Habari za uponyaji wake zikaenea katika kisiwa chote na kwa hio kila alie na mgonjwa alimleta kwa Paulo kumponya (Matendo 28)*

*Kama mtu yeyote anaumwa, itamlazimu kumpeleka kwa kiongozi wa kanisa ili kumpake mafuta na kusema kwa jina la Baba Mkuu na kuombea akuponyeshe. Maombi ya Imani kuiponya mgonjwa (James 5 : 14 - 15)*

## Mathayo 14 : 34 - 36

Yesu alikuja katika nchi ya Genesareti. Watu walipomuona na wakamtambua, habari zake zikaenea nchi yote, na kumletea wagonjwa na kumuomba tu wakamate nguo yake nao wote waliokamata nguo waliponyeka.



Mnamo tarehe 14 Feb 2012, mfungwa maombi kwa ajili ya mama yake aliekuwa matatizo ya kuziba mishipa ya damu, ikabidi kupelekwa hospitalini na siku inayofuata kufanyiwa operesheni.
Yule mfungwa alimuomba Yesu ampatie moyo wa ujasiri na kwa vile hakuwa mtaalamu wa kuomba ila kwa vile aliomba msaada kwa Yesu, siku ya pili kwa vile alikua na bidii ya maombi. Mnamo tarehe 16 Feb yule mfungwa alipokea habari toka kwa dada yake kwamba “Mama yuko mzima, na wala haitaji operesheni tena na amerudi nyumbani yuko mzima wa afya.”

## Mathayo 18 : 19 - 20

Yesu aliwaambia wanafunzi wake,
"na waambieni kwa uhakika
ikiwa wawili wenu watapatana kwa
jambo lolote hapa duniani
watakaloliomba kwa Baba
yangu aliembiguni kwakua.
walipo wawili au watatu
wamekusanyika
kwa jina langu
na mimi nipo kati yao."




*Siku moja saa tisa na nusu mchana John na Peter walienda kuomba kanisani. Maskini aliwaomba pesa nae. Alikua kilema wa kuzaliwa. Peter alimwambia yule kilema "Sina kitu cha kukupa, sina fedha wala dhahabu, ila nina kitu cha kukupa : kwa jina la Yesu Kristo wa Nazareti, simama na utembee."*

*Peter alimshika mkono yule kilema, na kumsaidia kusimama, hatimae alisimama na kuanza kutembea, alikua na furaha sana, alianza kuruka ruka akitembea huku na kule na kumtukuza Mungu (Matendo 3)*

## Mathayo 15 : 21 - 28

Wakati Yesu alipokwenda katika eneo moja karibu karibu na Tyre na Sidoni. Wanawake wa Cannanite walianza kupiga kelele na kuita "Wewe mwana wa Daudi, tuhurumie. Mtoto wangu anasumbuliwa na shetani." Yule mama alipiga magoti na kumuomba Yesu amsaidie. Yesu akamwambia yule mama "Imani yako iko imara." Na mpaka hivi sasa mtoto wako. amesha ponya na yuko mzima.




------------------------------------------

*Mara kwa mara Yesu aliwaponya watu, alikua akisali kwa Imani. Ikiwa imani yetu ni imara, Yesu atatusaidia. Nikama mtu ambae anajifunza kuogelea, akiweka imani kwa mwalimu wake, hatimae atajua kuogelea. Kwa upande mwengine kama huna imani huwezi kuogelea*



*Bwana Yesu tafadhali niongozee Imani!*

Mathayo 15 : 29 - 31

Karibu na pwani ya Ziwa Galilaya, alipanda mlimani na kuketi, kundi la watu wenye ulemavu, viwete, mabubu, vipofu. Walimuendea na kukaa chini ya miguu yake, Bwana Yesu aliwaponya wote. Watu walistaajabu kuona bubu anasema, viwete wanasimama, vilema wanatembea, vipofu wana ona. Kila mmoja alimtukuza Mungu.



*Sam alianza kutumia madawa ya kulevya wakati akiwa na umri wa miaka 14 na kupelekwa kituo cha matibabu zaidi ya mara sita. Alikua akienda na kurudi kila mara. Na baadae kuomba bwana Yesu "Yesu nisaidie." Tokea wakati huo hakuwahi kurejeshwa tena kwenye matibabu. Kitabu cha "Chasing Dragon" by Jackie Pullinger kimeelezea habari mbali mbali kuhusu Sam uvutaji. Wa madawa ni ushawishi wa shetani. Bwana Yesu pekee ndie anaeweza kutuzuia kutokana na ushawishi wa Shetani*

Waumini walikusanyika katika hekalu. Miujiza mingi ilifanyika, watu wagonjwa walilazwa mitaani ili Peter akija kivuli chake kiwa funike wakati akitembea. Watu walifika kutoka miji ya pembezoni ya Yerusalemu wakileta wagonjwa wao. Wagonjwa wote walipona (Matendo 5)

*Philipo alitangaza na kuhubiri habari za Yesu katika mji wa Samaritan. Wasamaria waliupokea ujumbe wa Philipo kwa sababu ya miujiza aliokua akiifanya. Watu walitolewa mapepo machafu, idadi kadhaa ya viwete waliponywa. Miujiza ile ile ilileta furaha kubwa katika mji ule* (Matendo 8)

Peter alitembelea makanisa mengi katika mji wa Luda, na akakutana na mtu anaitwa Aeneas ambae amepooza kwa muda wa miaka 8 amelala kitandani.
Peter akamwambia
"Aeneas, Yesu amekuponya."
Alinyanyuka na kufunga kitanda chake na akanyanyuka mara moja.
Watu wa eneo lile wakabadilika
na kuwa watu wa Mungu. (Matendo 9)

Mathayo 17 : 14 - 20

Yule jamaa alipiga magoti kwa Yesu na kusema “Bwana nihurumie mtoto wangu. Ana matatizo ya akili na maisha yake ni Kila siku anakuwa anaanguka ndani ya moto au maji. Nilimpeleka kwa wanafunzi wako wakashindwa.”
Yesu akasema “Mlete hapa huyo kijana.”
Yesu akamkemea yule shetani,
na yule shetani akatoka kwa yule kijana,
na akawa mzima toka wakati ule.
Baadae wanafunzi wakamuuliza Yesu
“Kwa nini tumeshindwa kumfukuza shetani kwa yule kijana?”
Yesu akajibu
“Imani yenu bado haijakuwa imara sana.”





Njia moja ya kuomba kwa pamoja na marafiki ni kila mmoja kuweka mkono wake wa kulia kwenye bega la kushoto la mwenzake, unapofanya hivyo hisia za uponyaji, kutoka katika mkono wako wa kulia na bega la kushoto pamoja na moyo, na kama sehemu zako za mwili haziko mzima, basi hisia zile zitaamsha zile sehemu na kuwa imara. Kuomba kwa pamoja mara nyingi, kunaleta uponyaji kuliko kuomba kwa watu wawili, lakini sio kama kuomba kwa pamoja siku zote kunafaa, lakini imependekezwa sana. Fikiria kwamba mkono wa kulia kama vile mkono wa.....Yesu

Mathayo 7 : 11 - 17

Siku moja Yesu na marafiki zake walienda mji mmoja unaitwa Nain. Muda mchache baada ya kuingia katika mji ule, jamaa mmoja ambae alikua amekufa, alikuwa wanampitisha kwa ajili ya kuenda kumzika, na yule mama mjane alikuwa analia na kusema "ni mtoto wangu pekee."
Yesu moyo wa imani ukamjia akaenda na kumwambia "ee mama usilie," na kumpoza.
Yesu akasema na yule kijana ambae amefariki.
Akamwambia we "kijana nakwambia Simama." Yule jamaa ambae amefariki akasimama na kuanza kuongea, na Yesu akampelekea yule mama mtoto wake.



Moja katika sala bora ni sala ya uponyaji ni “sala ya Baba yetu”

Inatupasa tuisali kwa utaratibu na uangalifu na si haraka.

Yatupasa kutafakari maneno ya sala hii. “Baba yetu” na si “Baba yangu” kwa sababu Yesu ni mtoto mpendwa wa Mungu ni ndugu yetu atatuombea kwa Mungu.

Hivyo Nikiomba kwa mtu
ambae ni mgonjwa na sali hivi :

Yesu mponye Adam
Tafadhali Bwana mponye
Yesu naomba pamoja nawe mponye Adam :

*Baba yetu ulie mbiguni*
*Jina lako litukuzwe*
*Ufalme wako uje*
*Mapenzi yako yatimizwe hapa duniani*
*kama huko mbiguni*
*Utusamehe makosa yetu kama*
*tunavyo wasemehe waliotukosea*
*Usitutie majaribuni,*
*utulinde na maovu*

Luke 17 : 11 - 19

Siku moja Yesu alikwenda kijijini, watu wenye ukoma walifika kwake na kumwambia “ee bwana tuhurumie” Bwana Yesu aliwajibu “ee nendeni mkajioneshe kwa makuhani.” Wakati walipokwenda huko, walipona ukoma. Mmoja wao alirudi kwa Yesu akiwa na furaha, akaanguka kifudi fudi miguuni kwa Yesu na kumshukuru. Lakini Yesu alihudhunika kwa sababu wale wengine 9 hawakurudi kwake na kumshukuru.





Wakati mwengine mtu huzungumza, au elezea habari ya ugonjwa wake kwa wauguzi, familia, na marafiki wa karibu.
Wakati mwengine mgonjwa huzungumza kila mara kuhusu ugonjwa wake kwa watu mbali mbali. Kila wakati huzungumza vikwazo juu ya ugonjwa huo njia bora ni kuvipuuza vikwazo hivyo. Fikiri mara chache juu ya ugonjwa na mara zaidi juu Ya Bwana. Yesu ndie mponyaji au daktari mkuu (c.f. *God at Eventide* July 20)

Mnamo Feb, 2012 Mfungwa mmoja alilazwa katika Queen Elizabeth Hospital, kutoka na utumiaji wa madawa ulisababisha uvimbe katika mguu wake wa kulia chini ya goti.
Baada ya kupewa kitabu cha "Daktari Yesu" juu ya 18 Feb usiku alimuomba Bwana Yesu.

Siku iliofuata uvimbe wote ulitoweka na siku iliofuata akawa anatembea kama kawaida.
Miezi kadhaa iliyopita alipata tatizo lile lile katika mguu wake wa kushoto. Hospitali ile ile, dawa zile zile...uvimbe ulichukua miezi kadhaa. Uvimbe katika mguu wa kulia ulichukua siku mbili. Yule mtu alisema tafauti ilikuwa ni maombi kwa Bwana Yesu


---

Wakati Maria alipokuwa mjamzito, mama mkwe wake akamwambia "kama utajifunguwa mtoto wa kike, basi mtoto wangu atakuacha."
Maria akawa na wasi wasi juu ya jambo lile na ikasababisha mtoto akazaliwa mgonjwa, ambae hauwezi kutibika. Padri akamwambia Maria omba, "Tafadhali Yesu nisamehe mimi na Mama mkwe wangu." Na siku chache mtoto akapona.
Utusamehe hasa kwa wale ambao hawana mioyo au nia ya kuwasamehe sisi na huo ni ufunguo wa kuponya

Yesu, tafadhali nisaidie mimi kusamehe wale watu ambao hawana mioyo wa kuwasamehe mimi

Luke 18: 35 - 43

Yesu alikwenda katika mji mmoja unaitwa Jericho. Yule Kipofu anaomba barabarani. Yule kipofu alisikia kama yesu anapita, yule kipofu akaita “Ee Yesu, mwana wa Daudi, nihurumie!” Watu wengine wakamwambia yule kipofu nyamaza, lakini yule kipofu alizidi kuita kwa sauti, “mwana wa Daudi, nihurumie!” Yesu alimuuliza yule kipofu “nini unataka?” Yule kipofu akajibu, “Nataka kuona.” Yesu akamwambia “ona, Imani yako imekuponya.” Na imekusaidia Muda mchache. Yule kipofu akaona na baadae akamfuata Yesu, huku akimtukuza kwa sauti kubwa



Muheshimiwa daktari : huo uwezo wako wa kuponya ni zawadi toka kwa Baba Mungu (Sirach 38 : 1 - 4)




Wakati mwengine watu wanasema kuwa “hawajui jinsi gani ya kuomba”. Lakini kuomba hakuna ugumu wowote kwani kuomba ni mazungumzo kati yako na Yesu kama rafiki. Wala huhitaji kusema maneno mengi ili Yesu aelewe, bali hata maneno kidogo yanatosha. Yesu anaelewa yote yalioko moyoni mwako. Wala huhitaji sherehe aina yoyote, kwa maana Yesu sio kiziwi. Wewe sema maneno kidogo tu na kuamini Yesu atasikia, kama vile mtoto anapoongea na baba yake au mama yake.

Yesu tafadhali nisaidie kuomba
na unisaidie kuongea na wewe

## Mathayo 20 : 29 - 34

Wakati Yesu anaondoka katika mji wa Jericho, vipofu wawili walikuwa wamekaa njiani. Waliposikia Yesu anapita, walimuita kwa kelele, wakisema "ee mwana wa Daudi tuhurumie." Watu waliokuwa karibu walikasirika na wakawaambia wale vipofu wanyamaze kumuita Yesu, lakini wale vipofu walipinga na waliende lea kumuita Yesu tena kwa sauti kubwa zaidi. Yesu alisimama na kuwaita na kuwauliza "mnasemaje?" Wale vipofu waka jibu "ee Bwana tunataka kuona". Yesu aliwahurumia na akawagusa macho yao. Mara wakarudia kuona na wakaanza kumfuata Yesu.





Maombi mazuri kwetu “ni kuwekewa mikono”: na kusema Yesu mponyeshe (fulani) jaza mapenzi yako kwake, mapenzi yako ya tampatia, matumaini yamtie nguvu kuwa shujaa na kusamehe, pamoja na amani na uponyaji wa mwili, akili na kiroho.



Mathayo 21 : 12 - 14

Yesu alipoingia katika mji wa Jerusalem. Watu walimkaribisha kwa kupungia kwa matawi ya majani ya mitende. Yesu akaenda kwenye nyumba ya ibada “hekalu” na kuwafukuza wabadilisha pesa pamoja na njiwa. Vipofu na vilema waliombewa na wakapona





*Kuna wakati baadhi ya magonjwa hutokana na historia ya mtu au ugonjwa wa kurithi. Hii inatokana mara kwa mara zaidi ya mtu mmoja kuugua ugonjwa wa aina moja katika familia. Bwana Yesu ni bwana wa historia na wakati. Analeta amani na uponyaji katika familia zetu, huponya magonjwa ya kurithi katika familia.*

*Hiki ni kitabu cha Dr. Kenneth McAll :*

- *Healing the Family Tree*
- *A Guide to Healing the family tree*

Bwana Yesu ikiwa mmoja wetu, au hali yoyote ipo katika familia yetu, sasa nakuomba uiondoshe hali hio. katika ukoo wetu au familia yetu. Naomba pamoja nawe : Baba yetu ulie mbiguni.....

## Historia ya muhinu wa kuiombea familia zetu

Mwanamke mmoja mwenye umri wa miaka 50 alikua akisumbuliwa na ugonjwa Parkinson's Disease. Ugonjwa wa kutetemeka hakuweza kupata usingizi kwa zaidi y masaa 24 zaidiya kutetemeka. Yeye na mume wake walitumia pesa nyingi lakini dawa za Kichina na Magharibi hazikuweza kumsaidia


Hivyo mwanamke alimuomba mchungaji amsaidie. Mchungaji kwa unyenyekevu alimuuliza yeye na mume wake kuhusu historia ya familia zao. Kama kuna jambo lolote lisilo furahisha ambalo limetokea katika miaka ya karibuni, vitu kama vile : mauaji kuharibika mimba, kutoa mimba, ajali mbaya za barabarani nk. Yawezekana mtu hakua na amani na anahitaji maombi

Mke na mume walisema kwamba kabla ya mtoto wao wa kwanza kuzaliwa, walitowa mimba 2. Baada ya mtoto wa pili kuzaliwa wakatoa mimba 2. Mchungaji alitaka kupatiwa majina ya watoto 4. Wawili wa kiume na wawili wa kike, ingawa jinsia za watoto hawa hazikufahamika. Mchungaji aliwataka mke na mume kuomba msamaha watoto hao na wauguzi wa hospitalini

Mchungaji aliwataka mke na mume kumuomba Bwana Yesu watoto hao wapumzike kwa Amani, na kwamba wazazi na watoto wao watakutana mbiguni. Siku chache baada ya maombi hayo. yule mwanamke alipona ule ugonjwa wa kutetemeka

Luke 22 : 50

Yesu alijua kuwa muda wa kufariki umekaribia. Alikula chakula cha mwisho na marafiki zake, basi walipokwenda kuomba katika bustani. Wakati wa kuomba, kundi la watu walikuja kumkamata. Peter alitoa upanga na kumkata sikia la kulia, mmoja wapo katika kundi liliomkamata Yesu. Yesu alipomwambia Peter rudisha upanga wako ndani. Yesu alikamata lile sikio na kumponya



*Hata ule muda Yesu amekamatwa, bado alikuwa anaendelea kuponya watu, na aliendelea kuponya pamoja na kukamatwa kwake Yesu, lakini bado alikuwa anawaonea huruma wagonjwa, na alikuwa anapenda kuwaponya wagonjwa. Hakuna hata mmoja alie sikitika zaidi kuliko Yesu wakati mtoto mchanga anapofariki. Dunia yetu ndio kwanza inatambua uponyaji wa Yesu.*


Yesu tafadhali niongezee mapenzi ya uponyaji

Katika magereza kulikuwa na habari nyingi zinazohusu uponyaji, ambao wengi wao wamefanikiwa :

Mnamo mwezi wa March 23, 2012 :
Mfungwa mmoja alituomba, tumuombee kuhusu kaka yake ambae alikua mgonjwa sana, karibu ya kufa, baadae wafungwa walimuombea yule kaka yake ambae yuko Africa, na baada ya wiki moja walipokea habari kwamba yule kaka yake yuko mzima bila matatizo.
Yoyote wafungwa walimshukuru :
"MUNGU NI MWEMA!"

Yesu aliponyesha watu muda mrefu uliopita, kwa hio anajua aina zote za magonjwa duniani, uponyaji wa Yesu bado unaendelea hadi leo hii, kwa sababu uponyaji wa Yesu uko wazi kwa kila mtu anaetaka, basi atapata popote alipo
Furusa ya kuingia ni, kuomba hivi :
"Yesu tafadhali nisaidie. Yesu tafadhali niponye"

Kitabu hiki pamoja na habari za uponyaji utaikuta katika tavuti www.doctorjesus.org
Kama unataka kuweka habari ya uponyaji katika hii tavuti. Tafadhali tuma maoni barua pepe jdwomi@gmail.com






Mimi sina miguu
Mbinguni utakuwa na miguu

Mimi ni kipofu na kiziwi
Mbinguni utaweza kuona na kusikia

Mwili wangu wote umeungua na moto
Mbinguni hautakua na alama yoyote

Nimezaliwa taahira
Nimezaliwa na ugonjwa wa kuanguka
Mbinguni utakuwa mzima wa afya njema

Msalabani mwili wa Yesu ulikuwa
na alama ya misumari.
Baada ya siku tatu alifufuka
na mwili wake ulikuwa mzuri bila ya alama
yoyote, marafiki zake hawakuweza kumtambua

Watu wenye matatizo ya ulemavu na akili
watakuwa wazima Mbinguni kama Yesu

*Katika miaka 2000 iliopita*
*Yesu aliwaponya wagonjwa wa :*
*viziwi, mabubu, vipofu, viwete na wakoma.*

*Tokea wakati ule hadi leo hii,*
*watu wanapona wanao kuomba wewe.*

*Yesu mimi mgonjwa tafadhali niponye*
*Yesu tafadhali mponye rafiki yangu*

Kwa muda wa miezi 3 nilikua na maumivu ya kifua, na hakuna dawa ilionisaidia. Na baadae usiku mmoja wakati nasoma kitabu cha "Daktari Yesu" na nilimuomba Yesu msaada na asubuhi yake hakuna maumivu
- ni mfungwa alieko Hong Kong, Nov 11, 2011

Watu wamesaidiwa na "Daktari Yesu"
na pia wamesaidiwa na "Simple Bible"
Tovuti www.simplebible.info

Illustrations : Edmund
ISBN 978-988-12396-9-3
First printing, December 2014
Printed in HK by Print Shop www.printshop.hk
For private distribution only.    Not for sale
Published in HK
by Fr John David Wotherspoon OMI 胡頌恆神父
Email: jdwomi@gmail.com    Tel: (852) 67095674
This book is available in many languages
God bless kind friends who produced this book